## 4.0 KISWAHILI (102)

### 4.1 MATOKEO YA MTIHANI WA KISWAHILI

MANYAM FRANCHISE
Discover!Learn!Apply

Jedwali linalofuata linaonyesha matokeo ya mtihani wa Kiswahili ya miaka ya 2003 hadi 2006

**Jedwali 4:** **Matokeo ya Kiswahili (102) ya Miaka ya 2003 Hadi 2006**

| Mwaka | Karatasi | Watahiniwa | Alama Ya Juu | Alama Ya Wastani | Alama Ya Tangamisho |
|---|---|---|---|---|---|
| **2003** | 1 | | 40 | 18.81 | 6.77 |
| | 2 | | 80 | 36.87 | 11.67 |
| | 3 | | 80 | 42.99 | 13.31 |
| | **Jumla** | **204,428** | **200** | **98.15** | **27.09** |
| **2004** | 1 | | 40 | 16.54 | 6.67 |
| | 2 | | 80 | 27.78 | 11.47 |
| | 3 | | 80 | 37.25 | 13.18 |
| | **Jumla** | **221,286** | **200** | **81.54** | **26.00** |
| **2005** | 1 | | 40 | 20.25 | 6.37 |
| | 2 | | 80 | 34.08 | 10.61 |
| | 3 | | 80 | 37.57 | 14.01 |
| | **Jumla** | **259,301** | **200** | **91.89** | **26.00** |
| **2006** | 1 | | 40 | 15.31 | 7.68 |
| | 2 | | 80 | 40.60 | 11.80 |
| | 3 | | 80 | 48.48 | 14.63 |
| | **Jumla** | **241,972** | **200** | **104.39** | **29.00** |

Jedwali hili laonyesha kuwa:

(i) Alama ya wastani ya karatasi ya kwanza (102/1) ya mwaka wa 2006 yamerudi chini kwa kiasi kikubwa yakilinganishwa na yale ya mwaka wa 2005.

(ii) Matokeo ya karatasi ya pili (102/2) ya mwaka wa 2006 yameimarika yakilinganishwa na yale ya mwaka wa 2005.Alama ya wastani imepanda kutoka ***34.08*** mwaka wa 2005 hadi ***40.60*** mwaka wa 2006.

(iii) Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2006 yameimarika yakilinganishwa na yale ya mwaka wa 2005 . Alama ya wastani ilikuwa ***37.57*** mwaka wa 2005 lakini ilipanda ikawa ***48.48*** mwaka wa 2006. Hii ni tofauti ya alama zaidi ya 10.

(iv) Kwa jumla matokeo ya Kiswahili ya mwaka wa 2006 yameimarika yakilinganishwa na yale ya miaka kadha iliyopita. Alama ya wastani ya mwaka wa 2006 iliweza kufika nusu ya alama zote zinazoweza kutuzwa, yaani 100. Alama hii ilikuwa ***104.39***. Kwa muda mrefu sasa alama hii haijafikia kiwango hiki.



Powered By: www.manyamfranchise.com

## 4.2 INSHA (102/1)

**Jedwali 5: Matokeo ya Karatasi ya Kwanza ya Miaka ya 2003 Hadi 2006**

| Mwaka | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 |
|---|---|---|---|---|
| Alama ya wastani | 18.81 | 16.54 | 20.25 | 15.31 |
| Alama ya tanganisho | 6.77 | 6.67 | 6.37 | 7.68 |

Jedwali hili laonyesha kuwa mwaka wa 2006 karatasi ya kwanza (102/1) ilifanywa vibaya zaidi ya miaka hiyo mingine mitatu tuliyochanganua. Alama ya wastani ilishuka kutoka ***20.25*** mwaka wa 2005 hadi ***15.31*** mwaka wa 2006. Hii ni tofauti ya karibu alama 10. Kwa sababu ya matokeo mabaya ya karatasi hii mwaka wa 2006, tumechanganua maswali yote ya insha huku tukieleza ni kwa sababu gani watahiniwa walikosa alama na yale majibu tuliyotarajia.

**Swala la Kwanza**

*Umeteuliwa kuwa katibu wa kamati inayotoa mapendekezo ya jinsi ya kupambana na tatizo sugu la dawa za kulevya. Andika ripoti yako.*

Hii ilikuwa ni insha ya kikamilifu ya kuandika ripoti. Watahiniwa wengi walishindwa kutumia mbinu ya kuandika wakionyesha hali ya maisha ya kila siku. Walibaki kuandika mambo ya kinadharia. Uandishi wa kikamilifu lazima unahusishwa na hali ya maisha ya kila siku. Insha hii ilitakikana iandikwe hivi ambavyo tumeonyesha hapa.

**Muundo.**

(i) Kichwa

- Kiteuliwe kulingana na mada husika.
- Kitaje mada na tarehe. (muda ambao kamati ilifanya kazi).
- Kiandikwe kwa herufi kubwa na kipigiwe mstari. (Udhaifu ushughulikiwa ki-mtindo).

(ii) Utangulizi

- Mwandishi atoe usuli mfupi au maelezo ya jumla kuhusu mada ya ripoti au historia fupi ya shughuli husika.

(iii) Mwili

- Uelezee maudhui, ripoti itumie nafsi ya tatu, kauli ya kutendewa na wakati uliopita.
- Inaweza kuwa na visehemu vyenye vichwa vidogo vidogo.

(iv) Hitimisho

- Alipotumia wakati au nafsi aondolewe zw(wakati) hapo mwisho baada ya kutuza.
- Aeleze japo kwa ufupi mambo muhimu katika ripoti. Aweza kutoa ushauri au mapendekezo kuhusu mada iliyoshughulikiwa kwa kuagiza mambo ya kufanywa au kukataza yasiofaa kufanywa.

(v) Jina la mtayarishi, sahihi na tarehe. (siku ya kuandika ripoti)
Kwa mfano:
Muundo wa ripoti uzingatie



Powered By: www.manyamfranchise.com

(a) Utangulizi: kichwa: kupambana na dawa za kulevya
(b) Dawa za kulevya

- Dawa ambazo zina athari mbaya kwa afya;
- Dawa zinazotumiwa vibaya;
- Dawa zenye athari ya uraibu: mairungi, mihadarati, bangi, sigara, pombe.

(c) Athari zake:

- Huathiri afya ya mtumiaji;
- Hujenga uraibu mbaya;
- Huathiri utenda kazi wa mtumiaji;
- Huwa chanzo cha mabadiliko ya kitabia;
- Huuharibu ubongo wa mtumiaji;
- Humzuga/humtawala mtumiaji kiasi cha kutoweza kufanya lolote bila kuzitumia;
- Huwa na athari kwenye jamaa na jamii;
- Huwa chanzo cha maovu mengi ya kijamii.

**Mapendekezo:**

- Uelimishaji wa jamii kuhusu madhara yake;
- Kutumia vyombo vya habari kama redio na runinga;
- Matumizi ya mabango katika maeneo mbalimbali;
- Kuhusishwa kwa elimu inayolenga madhara yake katika mtaala;
- Kuandaliwa kwa semina za kuhamasisha umma;
- Kusambazwa kwa maandisi ambayo yanalenga kuwaelimisha wanajamii;
- Kutumiwa kwa vyombo vya sheria;
- Kupambana na watumiaji;
- Kuwepo kwa vituo vya kuwasaidia walioathirika na dawa za kulevya;
- Kuwahusisha wananchi wote kwenye harakati za kupambana;
- Kuhusishwa kwa asasi kama dini (makanisa, misikiti n.k) kueneza habari hizi muhimu;
- Kuwepo na nyenzo za kuchunguza na kupambana na dawa za kulevya.

(d) Hitimisho: Makubaliano ya kikao
(e) Kitambulisho sahihi, hina na terehe.

**Swali la Pili**

*Ukubwa ni jaa.*

Watahiniwa walitakikana waandike insha ambayo ingeonyesha ukweli wa methali hii. Wengi walipotoka kabisa kwa kuongeza herufi ***"n"*** katika neno ***"jaa"*** likawa ***"njaa".*** Kufanya hivi kuliwafanya wapotoke kabisa katika insha zao. Waliofanya hivi walijitungia swali ***"ukubwa ni njaa,"*** na wakakosa alama kabisa.

**Majibu yaliyotarajiwa**

Mwelekeo insha iliyotarajiwa kuchukua;

Insha iakisi maana ya ndani ya methali kuwa cheo au mamlaka huwa ni kama mahali pa kutupa takataka. Maana ya ndani: mwenye cheo hulaumiwa au kushutumiwa mambo yanapoenda kombo. Wenye vyeo wasishangae wanapokumbwa na lawama kutokana na hali au matendo fulani.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Mtahiniwa aandike kisa kuthibitisha ukweli wa mêthali. Atakayeengemea upande mmoja atakuwa amepungukiwa - maudhui. Maelezo: ukubwa - cheo, mamlaka, umri, wadhifa, usimamizi, majukumu. JAA - kulaumiwa, kusingiziwa, kutusiwa, kutumiwa, kushutumiwa, kupigwa, kupigwa vita.

**Swali la Tatu**

*Malizia kwa ... Wekundu wa uchwejua ulienea kila mahali ; anga nzima ilijaa wekundu kama kwamba mazingira yalipatana na hali iliyokuwako. Kwa mbali nilisikia sauti iliyonikumbusha maneno niliyoambiwa zamani. Laiti ningeyasikiliza maneno hayo.*

Hii ni insha ambayo ilihitaji ubunifu na uwezo wa kufikiri haraka na kutunga kisa ambacho kingeoana na maelezo na ambacho kingeonyesha hali ya vidokezo vilivyo tolewa. Wanafunzi wengi hawakufuata maagizo na wakabaki kujiandikia mambo yao, na kupachika maneno ya vidokezo huko mwisho wa insha zao.

**Mwelekeo uliotarajiwa:**

Insha ya kiubunifu ambayo inapima uwezo wa mwanafunzi wa kubuni na kutunga kisa ambacho kinaingiliana na vidokezo vilivyotolewa.

**Sifa za kuchunguza:**

Insha iakisi sifa zifuatazo: majuto, maonyo. Yalihusu nini, aliasi namna gani, kwa nini akapuuza maonyo. Matokeo ya haya mapuuza . Athari za haya mapuuza:

(i) Asiyemaliza kwa maneno aliyopewa amejitungia swali na kulijibu.
(ii) Anayeongewa zk (kimalizio) baada ya kutuzwa.
(iii) Anayeanza kunakili kimalizio na asilamili aondelewe zk (kimalizio) baada ya kuuzu.

**Swali la Nne**

*"Utandawazi una athari mbaya katika maisha yetu". Jadili.*

Hii insha ilihitaji watahiniwa wawe na ujuzi wa maswali ibuka ambapo wengi hawajapata mwangaza wa kutumia kuweza kuyaelewa maswala haya.

**Majibu yaliyotarajiwa**

**Insha ya mjadala.**

Utangulizi: Utandawazi au utandaridhi:

- Mahusiano ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa teknolojia yanayokiuka mipaka ya kitaifa na kuufanya ulimwengu kuwa kama kitu kimoja/kijiji kitandaridhi/kitandawazi.

Faida za utandawazi

- Kuhimiza maingiliano ya jamii mbalimbali ulimwenguni.
- Kusambaza maarifa kutoka sehemu moja hadi nyingine.
- Kuwa msingi wa elimu na uenezaji wa maarifa muhimu.
- Kuchangia katika kusambaza haki au maarifa ambayo hayapatikani kwingineko.
- Kuharakisha maendeleo katika sehemu mbalimbali za ulimwengu.
- Kuwawezesha watu ulimwenguni kufaidika kutokana na teknolojia bora.
- Kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi ya maeneo mbalimbali kutokana na biashara kama utalii.
- Kuwa msingi wa ukuaji wa chumi mbalimbali - kutokana na biashara baina ya mataifa ya ulimwengu.
- Kuchangia kuwaelimisha raia kuhusu haki zao za kisiasa.



Powered By: www.manyamfranchise.com

- Huweza kuwa nyenzo muhimu katika kupanua elimu - matumizi ya mtandao kama msingi wa elimu.

Madhara ya utandawazi

- Uwezekano wa kusambaza tabia na tamaduni za kigeni zenye madhara mabaya kutokana na mtandao, runinga nk.
- Kuwepo kwa bidhaa zinazotoka mataifa mengine ambazo huathiri ukuaji wa viwanda vya nchini: kuna uwezekano wa kuamgamia kwa viwanda asili katika nchi zinazoendelea.
- Kusambazwa kwa imani ambazo hazifai au huweza kuwa na matokeo hasi katika jamii.
- Uwezekano wa mataifa makubwa yalioyoendelea kuumiliki ulimwengu: mashirika, kampuni na viwanda vyao ndivyo vilivyoendelea sana.
- Kukuzwa kwa matendo mabaya kama wizi wa watoto, ulawiti n.k. kutokana na kuwepo kwa mtandao ambao ni nyenzo/ wenzo muhimu ya utandawazi nk.
- Uwezekano wa kuichochea jamii dhidi ya serikali zao au jamii zao.
- Uwezekano wa jamii kutoendelea kutokana na uhamaji wa watu kutoka jamii moja hadi nyingine.
- Hali ya kudhibitiwa kwa mataifa machanga.

**Mapendekezo**

- Walimu waendelee kuwapa wanafunzi mazoezi zaidi katika uandishi wa kiuamilifu.
- Ni muhimu wanafunzi waelezwe kwamba ***"kujitungia swali"*** huwakosesha alama. Ni vizuri waangalie kichwa cha insha wakifikiri vizuri bila kuongeza mambo yao ambayo huwafanya wapotoke kimaudhui.
- Wanafunzi waelezwa kwamba insha ya kumalizia ni lazima ihusishwe na vidokezo vilivyotolewa. Mtu kujiandikia mambo yake kisha kupachika vidokezo hivyo mwisho wa insha ni makosa.
- Wanafunzi ni lazima wafunuliwe maswala ibuka katika upana wake wote ndiyo hata wao wawe mbele katika maswala yanayohusu ulimwengu wa leo.
- Insha ya mjadala ina sehemu mbili na mtahiniwa ni lazima aindike hivyo.

## 4.3 LUGHA (102/2)

**Jedwali 6: Matokeo ya Karatasi ya Pili (102/2) ya Miaka ya 2003 had 2006.**

| **Mwaka** | **2003** | **2004** | **2005** | **2006** |
|---|---|---|---|---|
| **Alama ya Wastani** | 36.87 | 27.78 | 34.08 | 40.60 |
| **Alama Ya Tanganisho** | 11.67 | 11.47 | 10.61 | 11.80 |

Matokeo ya karatasi hii ya pili (102/2) yametengemaa mwaka wa 2006. Alama ya wastani imeweza kufikia nusu ya alama zote ambazo zinaweza kutuzwa ambazo ni 80. Alama hii ilikuwa ***40.60*** mwaka wa 2006 jambo ambalo ni la kutia moyo. Tutachanganua maswali ya ufahamu na muhtasari tu kwa sababu ndiyo yaliyoelekea kuwatatiza watahiniwa.



Powered By: www.manyamfranchise.com

## Swali la 1

## Ufahamu

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

Ulimwengu unapaswa kuzuka na mbinu za kulitadarukia tatizo la umaskini ambao unakwamiza juhudi za maendeleo. Umaskini unaoyakabili mataifa yanayoendelea unayatosa kwenye dhiki kubwa huku mataifa ya kimagharibi yakipiga hatua kubwa kimaendeleo. Ufa uliopo baina ya mataifa yanayoendelea na yale yaliyoendelea kama vile Marekani, nchi za Ulaya na Ujapani unapanuka kila uchao.

Vyanzo vya umaskini huu ni anuwai mathalan, ufisadi, uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika, idadi ya watu inayoupiku uwezo wa uchumi wa taifa linalohusika na ukosefu wa nyenzo na amali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini. Ukosefu wa elimu na nafasi adimu za ajira huchangia pia katika tatizo hili.

Jamii ya ulimwengu inapaswa kuelewa kuwa umaskini unaoathiri nchi fulani una athari pana sana. Uvunjifu unaotokana na umaskini unaweza kuwa mboji ambako matendo mabaya huchipuka. Raia maskini huweza kushawishiwa haraka kujitosa kwenye matendo ya kihalifu ili kujinasua kutoka dhiki ile. Hii inaweza kuwa mbegu ya kuatika maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.

Mataifa ya magharibi yanapaswa kuyaburai madeni mataifa yanayoendelea kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipia madeni hayo. Katika hali hii inakuwa muhali kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na pingu za umaskini. Njia nyingine ni kustahabu kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi zinazoendelea.

Kwa upande wake, mataifa yanayoendelea yanapaswa kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini. Ni muhimu pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini. Pana dharura ya kuzalisha nafasi za ajira, kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tegemeo kuu la mataifa mengi, kuendeleza elimu na kuimarisha miundo msingi. Ipo haja pia ya mataifa haya kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru unaoutawala ulimwengu sasa hauishii kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umaskini zaidi. Kwa ufupi, maamuzi yote ya sera za kiuchumi lazima yauzingatie uhalisi wa maisha ya raia wa mataifa hayo.

Swali la ufahamu huhitaji uwezo wa mtahiniwa kusoma, kufahamu, kuchanganua, kusanisi, kufasiri na kutumia mawazo/dhana katika kifungu. Pia uwezo wa kuelewa matumizi ya msamiati maalum au kuweza jujieleza vizuri huhitajika. Swali la ufahamu mwaka wa 2006 lilihitaji stadi hizi zote. Watahiniwa nao walionyesha kukosa ujuzi wa stadi hizi muhimu wakabaki kuinua maneno kutoka kwa kifungu na kuyapachika hivyo hivyo yalivyokuwa bila hata kujaribu kujieleza.

### Swali la 1(a)

*Kwa nini umaskini umetamalaki katika mataifa yanayoendelea?*

### Majibu

- Ufisadi.
- Uongozi mbaya.
- Turathi za kikoloni.
- Uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika.
- Idadi ya watu inayoupiku uchumi wa nchi/taifa.
- Ukosefu wa nyenzo na amali za kukwamua raia kutoka lindi la umaskini.
- Ukosefu wa elimu.
- Nafasi adimu za ajira.
- Madeni.



Powered By: www.manyamfranchise.com

**Swali la 1(b)**

*Madeni yana athari gani kwa mataifa yanayoendelea?*

**Majibu**

- Hukwamisha/huzorotesha maendeleo.
- Huzidisha/huendeleza umaskini.
- Husababisha/huatika maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.

**Swali la 1(c)**

*Ni mapendekezo yapi ambayo mwandishi anatoa kwa mataifa machanga kuhusu utatuzi wa tatizo la umaskini?*

**Majibu**

- Kuwa na sera zinazotambua kuwa raia wengi ni maskini.
- Kuzalisha nafasi za ajira.
- Kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa.
- Kuendeleza elimu.
- Kuimarisha miundo msingi .
- Kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru hauui viwanda asilia.

**Swali la 1(d)**

*Mfumo wa soko huru una mathara gani kwa mataifa machanga?*

**Majibu**

- Ni chanzo cha kufa kwa viwanda asilia.
- Huendeleza umaskini.

**Swali la 1(e)**

*Ukirejelea kifungu, eleza maana ya:*

*(i)* *kulitadarukia*
*(ii)* *kuatika*
*(iii)* *kuyaburai madeni*

**Majibu**

i) Kulitatua/kulishughulikia/kulishuluhisha/kuliondoa/kulimudu/kulikabili.
ii) Kukuza/kuzalisha/kuanzisha/kupanda/kupandikiza/kuzua/kuleta.
iii) Kuyasamehe madeni/kuyafuta madeni/kuyaondolea madeni/kuyafeleti madeni/kuyabihi madeni/kutupilia mbali madeni.

**Swali la 2**

**Muhtasari**

Ajira ya watoto ni tatizo sugu linalokumba ulimwengu wa sasa, hasa katika nchi zinazoendelea. Jambo la kusikitisha ni kwamba hivi ndivyo ilivyo katika nchi nyingi za ulimwengu huu. Kuna idadi kubwa ya watoto wanaoajiriwa katika nyanja mbalimbali za jamii. Zipo sababu nyingi



Powered By: www.manyamfranchise.com

zinazowasukuma watoto kutafuta ajira barani Afrika kwa mfano, familia nyingi huishi maisha ya ufukara hivi kwamba hushindwa kuyatimiza mahitaji muhimu hususan kwa watoto. Kupanda kwa gharama ya maisha kunazidisha viwango vya umaskini. Ukosefu wa lishe pia huwafanya watoto kutoroka nyumbani kutafuta ajira. Janga la UKIMWI limesababisha kuwepo kwa idadi kubwa ya mayatima wanaoishia kutafuta ajira ili kuyakimu maisha. UKIMWI umezifanya familia nyingi pia kuwaondoa watoto shuleni ili waweze kuajiriwa kwa lengo la kuzalisha pato la familia hizo. Watoto wengine hutoroka makwao kwa sababu ya maonevu. Maonevu haya ni kama vile kupigwa, kutukanwa kila wakati, kunyanyaswa kijinsia na kadhalika. Huko nje hutaabishwa kimwili na kiakili. Hufanyishwa kazi za sulubu zenye malipo duni au wasilipwe kabisa. Hili huwasononesha na kuathiri afya yao.

Wengine hujiingiza katika vitendo vya jinai pale wanapokosa ajira. Huchukua sheria mikononi mwao, wakaendeleza vitendo vya ukatili kama vile kuwahangaisha watu na kupora mali yao au hata kuwakaba roho. Aidha, wengine hujikuta kwenye madanguro ambako huendesha biashara haramu.

Uundaji wa Umoja wa Afrika hivi majuzi ni hatua muhimu ya kushughulikia matatizo ya Afrika kama vile ajira ya watoto, kuzorota kwa miundo msingi, magonjwa, njaa, umaskini, ufisadi na ukabila. Katika kushughulikia haki za watoto, nchi za Afrika hazina budi kuzingatia masharti yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watoto. Nchi nyingi za Afrika ziliidhinisha mkataba wa masharti hayo, ikiwemo nchi ya Kenya. Nchi hizi basi lazima zishughulikie haki za watoto kupitia sheria za nchi. Watoto ni rasilmali muhimu na ndio tumaini la kuwepo kwa kizazi cha binadamu.

Swali la muhtasari huhitaji mtahiniwa asome, aelewe, achanganue, asanisi na kufanya muhtasari wa yale aliyosoma katika mtiririko unaofaa.

Muhtasari lazima ufanywe bila kupoteza hoja muhimu katika makala. Tatizo ambalo watahiniwa huwa nalo kila wakati ni kwamba hawana uwezo wa kueleza upya hoja muhimu katika makala wanayosoma. Hao huona rahisi kujaribu kuinua hoja moja kwa moja wakitumia maneno yale yale ya kifungu walichopewa. Wanapata shida kuungaisha hoja katika mtiririko unaofaa.

**Swali la 2(a)**

*Eleza mambo yote muhimu anayozungumzia mwandishi katika aya ya kwanza (maneno 45 - 50)*

**Majibu**

- Ajira ya watoto ni tatizo sugu ulimwenguni.
- Wengi huajiriwa katika nyanja mbalimbali.
- Familia nyingi huishi ufukarani.
- Kupanda kwa gharama ya maisha kunazidisha umaskini.
- Ukosefu wa lishe huwatorosha nyumbani.
- Ukimwi umesbabisha mayatima wengi.
- Ukimwi umesababisha watoto kuondolewa shuleni.
- Wengi hutoroka makwao kwa maonevu.
- Nje hutaabishwa kimwili na kiakili/hufanyishwa kazi sulubu/hulipwa malipo duni au hawalipwi.
- Hili huwasononesha na kuwaathiri kiafya.

**Swali la 2(b)**

*Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi, fupisha aya mbili za mwisho (maneno 50 -55)*



Powered By: www.manyamfranchise.com

**Majibu**

- Watoto wengine hujiingiza katika jinai wanapokosa ajira.
- wengine hujikuta madanguroni/huendesha biashara haramu.
- uundaji wa Umoja wa Afrika ni hatua ya kushughulikia matatizo ya Afrika.
- Nchi lazima zizingatie masharti ya Umoja wa Afrika kuhusu watoto.
- Nchi nyingi ziliidhinisha mkataba wa masharti hayo.
- Lazima zishughulikie watoto kupitia sheria za nchi.
- Watoto ni rasilimali na tumaini la kizazi cha binadamu.

Hizi ni hoja muhimu ambazo ilitarajiwa kwamba zingekuwa katika majibu ya watahiniwa. Hata hivyo, hoja hizi ni lazima ziunganiswe katika mtiririko unaofaa.

**Mapendekzo**

- Wanafunzi ni vyema wakielekezwa njia mwafaka za kujibu maswali ya ufahamu. Waelezwe kwamba ni lazima wasome kifungu kwanza na kujaribu kizielewa hoja muhimu na kuweza kuzieleza hoja hizo wakitumia maneno yao wenyewe.
- Walimu ni vizuri wawape wanafunzi wao mazoezi ya kutosha ya maswala ya ufahamu na kusahihisha huku wanafunzi wakielekezwa dhidi ya kuinua majibu moja kwa moja kutoka kifungo.
- Walimu waendelee kuwapa wanafunzi wao mazoezi zaidi ya kufanya muhtasari huku wakielekezwa namna ya kutiririsha majibu yao kwa njia inayofaa.
- Ingekuwa vyema walimu wakiwaeleza wanafunzi wao kwamba wakifanya muhtasari kwa kutumia maneno zaidi ya inavyotakikana huwa wanaondolewa alama.

## 4.4 FASIHI (102/3)

**Jedwali 7: Matokeo ya Karatasi ya Tatu (102/3) ya Miaka ya 2003 Hadi 2006.**

| Mwaka | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 |
|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 42.99 | 37.25 | 37.57 | 48.48 |
| Alama ya Tanganisho | 13.13 | 13.18 | 14.01 | 14.63 |

Jedwali hili laonyesha kwamba matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2006 yamekuwa Mazuri zaidi yakilinganishwa na ya miaka hiyo mengine mitatu iliyopita. Maswali ya ushairi peke yake ndiyo yaliyowatatiza watahiniwa kwa hivyo ndiyo yatakayochanganuliwa hapa.

**Swali la 6**

**Ushairi**

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

KWELI

1. **Neno la kweli daima, lina nguvu za kutosha**
**Ni silaha ilo nzima, shabaha kutopotosha**
**Neno ngome ya hishima, msema kweli hunyosha**
**La urongo lapotosha, dumu katika ukweli**

2. **Ukitaka taadhima, na hifadha ya kutosha**
**Uishi penye huduma, uwe ndiwe muongosha**
**Uwe mkweli daima, urongo wako ondosha**
**La urongo lapotosha, dumu katika ukweli**

3. **La kweli lina salama, *ghayati* linaridhisha**
**Lakinga mbele na nyuma, na kati lafurahisha**
***Hata kesini ungama, Mola atasahalisha***
**La urongo lapotosha, dumu katika ukweli**

4. **Ruhusa urongo sema, patatu nakujulisha**
**Ni kauli ya Hashima, wengi *wamesadikisha***
**Ni hadithi twaisoma, nasi tumejifundisha**
**La urongo lapotosha, dumu katika ukweli**

5. **Kwanza urongo useme, iwapo wapatanisha**
**Pili ni mke na mume, ili ndoa kudumisha**
**Na vitani usikome, ni haki kuhadaisha**
**La urongo lapotosha, dumu katika ukweli**

6. **Wasalamu kaditama, sitaki kuyarefusha**
**Waja wa leo si wema, si hoja kuwagutusha**
**Wathamini darahima, haki wakaziangusha**
**La urongo lapotosha, dumu katika ukweli**



Powered By: www.manyamfranchise.com

**Swali la 6(a)**

*Taja manufaa ya ukweli kama yalivyoelezwa na mshairi.*

**Majibu**

- -Ni silaha/kinga.
- -Ni ngome ya hishima/taadhima.
- -Ukweli huridhisha.
- -Ukweli hupatanisha.

**Swali la 6(b)**

*Taja na kutoa mifano ya tamathali mbili za usemi katika shairi.*

**Majibu**

Stiari: Haki kuziangusha

- Tashhisi - Lakinga mbele na nyuma
- Tabdila - hifadha

**Swali la 6(c)**

*Dondoa na ueleze mifano miwili tofauti ya uhuru wa kishairi katika shairi hili.*

**Majibu**

Ilo - inkisari
Muongosha, Kuhadaisha - tabdila
Hishima - lahja

**Swali la 6(d)**

*Andika ubeti wa tano katika lugha nathari.*

**Jibu**

Ni haki kudanganya kwanza unapopatanisha, pili unapotaka kuhifadhi ndoa au vitani. Katina miktadha mingine dumu katika ukweli.

**Swali la 6(e)**

*Eleza maana ya :*

*(i)* *ghayati*
*(ii)* *hata kesini ungama, mola atasahalisha.*
*(iii)* *wamesadikisha*

**Majibu**

(i) Kabisa
(ii) Ukiwa katika kesi tubu ama useme ukweli: mola atakusaidia.
(iii) Wamefanya wasadiki/Wamefanya waunge mokono



Powered By: www.manyamfranchise.com

**Swali la 7**

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

**MKULIMA**

**Mtazameni...nguzo ya Afrika**
**mtumwa wa watumwa waloridhiya!**

**Amekita jembe lake akilisujudia**
**kwa *tambo* liloumbuka na kuselehea**
**Uso ukifuka ukata ulojifanya tabia**
**na machungu ya maonevu alovumilia.**

**Moyo wake mzito *ulokokomaa* kama kuni**
**Haujui tena kutarajia wala kutamani**
**Umekufa ganzi, kutohisi raha wala huzuni**

**Basi iteni fikira mambo mukiyafikiri**
***Siku hamaki yake itapochafuka kama bahari***
**Siku ukweli wa hali yake utapodhihiri**
**Umejiandalia vipi...**
**huo mkono ulomuumbua na kumkausha**
**hizo pumzi zilomzimia taa ya maisha**
**kumfunga kizuizi, gizani *kumtowesha*?**

**Ni jawabu gani alowekewa na wakati**
***kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti***
**kuiliwaza hamaki ya njaa hii ya dhati**
**Njaa ya maisha itakayo kushibishwa.**

**Swali la 7 (a)**

*Eleza mambo muhimu yanayojitokeza katika shairi hili.*

**Majibu**

- Mkulima ambaye ni nguzo ya Afrika ni kama mtumwa.
- Anateseka, ana huzuni na hana matumaini
- Baadaye matumaini yanaweza kwisha
- Kuna siku ambapo atafahamu haki yake na aidai
- Wanaomtesa wataadhibiwa

**Swali la 7 (b)**

*Taja na utoe mifano ya aina zozote mbili za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi hili.*

**Majibu**

(i) Tashbihi: Kama kuni
Kama bahari
(ii) Kweli kinzani: Mtumwa wa watumwa waliyoridhiya
(iii)Tashhisi: Pumzi zilozozima taa za Afrika
Amekita jembe lake akilisujudia

**Swali la 7 (c)**

*Eleza umbo la shairi hili.*



Powered By: www.manyamfranchise.com

**Majibu**

- Beti tano.
- Mishororo haitoshani.
- Shairi huru.
- Vina vya nje vipo.

**Swali la 7 (d)**

*Onyesha umuhimu wa matumizi ya kihisishi katika shairi.*

**Majibu**

Mshangao, masikitiko kuwa aliye nguzo ya Afrika ni mtumwa wa watumwa.

**Swali la 7 (e)**

*Fafanua maana ya:*

(i) *Siku hamaki yake itapochafuka kama bahari.*
(ii) *kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti.*

**Majibu**

(i) Wakati atakapozinduka na kuidai haki yake.
(ii) Kutuliza hasira za matakwa/matatizo yake hata kama ni kidogo.

**Swali la 7 (f)**

*Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi:*

(i) *tambo*
(ii) *ulokokomaa*
(iii) *kumtowesha*

**Majibu**

(i) Umbo.
(ii) Uliokauka.
(iii) Kumwingisha/kumtopesha.

## 4.5 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

4.5.1 Matarajio kwa wanafunzi wa kidato cha nne katika uandishi wa insha ni ya juu. Inasikitisha kuona kwamba wengi wa watahiniwa bado wana ule mtindo wa shule za msingi wa kujaribu kuandika insha kwa kutumia maneno makubwa makubwa ambayo hayachangii mada ya insha. Ni vizuri wanafunzi wajue kuwa kiwango chao ni cha kuandika insha zinazotoa hoja kamili na kufuata mada inavyotakikana.

4.5.2 Watahiniwa wengi bado wana matatizo ya kujibu maswali ya kifungu na pia ya muhtasari. Ni vizuri waendelee kupewa mazoezi ya kujibu maswali ya stadi za juu katika fahamu ndio waweze kutayarishwa vilivyo. Maswali ya muhtasari huwasumbua kwa sababu wao wanapenda kuinua majibu moja kwa moja kutoka kwa kifungu. Shida hapa ni kwamba huku kuinua hakuwasaidi kufikiria juu ya hoja muhimu, na wakifanya hivi basi hoja zao huwa hazikamiliki. Mtiririko wa majibu pia unavurugika.

4.5.3 Ushairi bado unatatiza wanafunzi. Walimu jaribuni kuwatia moyo wanafunzi wenu kwamba ushairi si ngumu. Wafundisheni juu ya aina zote za mashairi na pia arudhi za ushairi, lugha inayotumika, tamathali n.k.



Powered By: www.manyamfranchise.com